TANGAZO LA SERIKALI Na. 1014 la tarehe 6/12/2024

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA),

(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153(1))*

SHERIA NDOGO YA AFYA, USAFI NA HIFADHI YA MAZINGIRA YA HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA YA MWAKA 2024

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

**1**. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Afya, Usafi na Hifadhi ya Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa ya Mwaka 2024

Matumizi

**2**. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa.

Tafsiri

**3**. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo:

"afisa mwidhiniwa" maana yake ni afisa aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"eneo la hifadhi" maana yake ni eneo la mlima, eneo la chanzo cha maji, hifadhi ya misitu, miteremko na maeneo mengine ambayo yatatangazwa na Halmashauri kuwa ni maeneo ya hifadhi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa;

Sura ya 191

"maji taka" itakuwa na maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira

Sura ya 191

"mazingira" itakuwa na maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

"mkazi" maana yake ni mtu anayeishi au kufanya kazi ndani ya eneo la Halmashauri na inajumuisha taasisi na kampuni;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya……..au afisa atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi cha watu, kampuni au taasisi iliyoingia mkataba kutekeleza jukumu lolote chini ya Sheria Ndogo hii kwa niaba ya Halmashauri.

## SEHEMU YA PILI
## AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA

Wajibu wa kufanya usafi

4. Kila mkazi atakuwa na wajibu wa -
(a) kuweka mazingira ya makazi na eneo la biashara katika hali ya usafi muda wote;
(b) kuwa na choo safi na imara kwenye nyumba au eneo la biashara analomiliki;
(c) kuwa na chombo imara chenye mfuniko kwa ajili ya kuhifadhia taka ngumu;
(d) kufanya usafi katika eneo analomiliki ambalo halijaendelezwa; na
(e) kushiriki katika usafi wa mazingira wa pamoja kwa siku na muda ambao umeainishwa katika sheria au miongozo itakayotolewa na Serikali.

Choo cha muda

5.-(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu, kikundi au taasisi yenye lengo la kukusanya watu kwa madhumuni ya mkutano, sherehe au mkusanyiko wowote kuweka choo au vyoo vya muda iwapo eneo hilo halina choo au vyoo.

(2) Mtu, kikundi au taasisi inayotaka kuweka choo au vyoo vya muda itatakiwa kuzingatia kanuni za afya, usafi na utunzaji wa mazingira.

(3) Afisa afya wa Halmashauri atawajibika kukagua na kuhakikisha kuwa uwekaji wa choo au vyoo umezingatia kanuni za afya, usafi na utunzaji wa mazingira.

Udhibiti wa mazalia ya mbu na

6. Kila mkazi atakuwa na wajibu wa kuhakikisha eneo analoishi au kufanyia biashara halina maji yaliyotuama,

wadudu hatarishi

maji taka, taka ngumu au kitu chochote ambacho kinaweza kuruhusu kuwepo kwa mazalia ya mbu au wadudu wengine wenye madhara kwa afya ya binadamu.

Usafi wa pamoja

7.-(1) Kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi itakuwa ni siku ya usafi wa mazingira wa pamoja na kila mkazi atawajibika kushiriki.

(2) Usafi wa mazingira wa pamoja utafanyika kuanzia saa 1:00 asubuhi hadi saa 4:00 asubuhi.

(3) Muda wote wa usafi wa mazingira wa pamoja shughuli zote zisizohusu usafi hazitafanyika isipokuwa huduma muhimu kama itakavyoelekezwa na Halmashauri.

Usafi wa mifereji

8. Kila mkazi atakuwa na wajibu wa kuhakikisha hatupi taka au kumwaga uchafu kwenye mifereji ya maji ya mvua inayozunguka au kupita kando ya nyumba anayoishi, eneo la biashara, kiwanja anachomiliki au eneo lingine lenye mfereji wa maji ya mvua.

Uhifadhi wa maji taka

9.-(1) Kila mmiliki wa nyumba, kiwanda au eneo la biashara atakuwa na wajibu wa-

(a) kuchimba shimo la maji taka au kuweka miundombinu ya kuelekeza maji taka kwenye mfumo rasmi wa maji taka;
(b) kuondoa maji taka katika shimo la maji taka mara linapojaa; na
(c) kutotiririsha au kutoelekeza maji taka kutoka katika choo, bafu, shimo la maji taka au kiwanda kwenda kwenye barabara, uchochoro, chanzo cha maji, eneo la wazi, mfereji wa maji au sehemu yoyote ambayo haijatengwa kwa ajili ya kuhifadhia maji taka.

Wajibu kwa wafanyabiashara

**10**.-(1) Mtu anayekusudia kufanya biashara atahakikisha anapata kibali kutoka Halmashauri na anafanya biashara katika eneo lililoruhusiwa kwa ajili hiyo.

(2) Itakuwa ni wajibu wa mtu-

(a) anayekusudia kuuza chakula cha aina yoyote kuzingatia masharti na kanuni za afya;

(b) anayefanya biashara ya vyakula vilivyopikwa au kukaangwa-
   (i) kuhifadhi vyakula kwenye sanduku lililotengenezwa kwa mbao safi au aluminiamu na kuwekwa kioo kuzuia vumbi na wadudu waletao madhara kwa afya ya binadamu; na
   (ii) kuweka vyakula juu ya meza wakati wa kuuza;

(c) anayefanya biashara ya matunda, mbogamboga au biashara nyingine kama hiyo kufanya biashara katika mazingira ya usafi;

(d) anayefanya biashara kuweka chombo maalumu cha kuhifadhi taka; na

(e) anayefanya biashara ya kupuliza dawa au kuua wadudu, kufanya biashara hiyo kwa namna inayolinda afya na kuhifadhi mazingira ya eneo husika.

Zuio la shughuli wakati wa magonjwa ya mlipuko

11. Mkurugenzi anaweza kutoa amri ya kuzuia shughuli yoyote kufanyika iwapo atakuwa na sababu ya kuamini kwamba shughuli hiyo inaweza kusababisha kuenea kwa magonjwa ya mlipuko na kuleta athari kwa maisha ya binadamu.

Upimaji wa afya

12. Kila mfanyabiashara, mmiliki au mhudumu wa hoteli, mgahawa, baa, nyumba ya kulala wageni, bucha, mwoka mikate, au mtu anayeshughulika na kuuza vyakula vilivyopikwa atahakikisha kwamba anapima afya kila baada ya miezi sita kwa madhumuni ya kulinda afya za wateja.

Eneo la kutupa taka

13. Halmashauri itakuwa na wajibu wa-

(a) kutenga eneo maalumu kwa ajili ya kutupa taka;
(b) kuweka vyombo vya kukusanyia taka katika maeneo ya umma;
(c) kutoa huduma ya uzoaji taka; na
(d) kuteketeza taka katika eneo lililotengwa kwa ajili hiyo.

Ada ya uzoaji taka

14. Kila mkazi anawajibu wa kulipa ada ya huduma ya uzoaji taka kwa Halmashauri kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika sheria ndogo inayohusiana na ada na ushuru iliyotengenezwa na Halmashauri.

Udhibiti utupaji wa taka kwenye vyombo vya usafiri

15.-(1) Kila mmiliki wa chombo cha usafiri wa umma ataweka chombo au kifaa maalumu kwa ajili ya kuhifadhia taka za abiria.

(2) Watumiaji wa vyombo vya usafiri binafsi au vya umma hawataruhusiwa kutupa taka nje ya vyombo hivyo.

(3) Mtu atakayekiuka masharti ya kanuni hii anatenda kosa.

Ukaguzi

16.-(1) Afisa mwidhiniwa anaweza kuingia katika jengo lolote kwa lengo la kufanya ukaguzi juu ya utekelezaji wa masharti ya Sheria Ndogo hii.

(2) Endapo baada ya ukaguzi, afisa mwidhiniwa atabaini upungufu katika utekelezaji wa masharti ya Sheria Ndogo hii, Mkurugenzi atatoa notisi ya muda usiozidi siku thelathini kwa mkazi kurekebisha upungufu uliobainika.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (2), Mkurugenzi anaweza kusitisha matumizi ya jengo ambalo mkazi ameshindwa kurekebisha upungufu uliobanika.

## SEHEMU YA TATU
## HIFADHI YA MAZINGIRA
### *(a) Masharti kuhusu ufugaji*

Wajibu wa Halmashauri

17. Halmashauri itakuwa na wajibu wa-

(a) kutenga maeneo maalum kwa ajili ya shughuli za malisho ndani ya eneo la Halmashauri;
(b) kutenga njia maalum ya kupitisha mifugo kwenda na kurudi kwenye malisho au minada;
(c) kufanya sensa ya mifugo na kutoa kadi za usajili wa mifugo; na
(d) kutoa elimu ya ufugaji bora kwa jamii.

Wajibu wa mfugaji

18. Mfugaji atakuwa na wajibu wa-

(a) kufuga na kulisha mifugo katika maeneo ya malisho yaliyotengwa na Halmashauri;
(b) kupitisha mifugo katika njia zilizopangwa au kutengwa na Halmashauri;
(c) kutokata miti; na
(d) kusajili mifugo katika rejesta ya kijiji.

Katazo kwa mfugaji

19.-(1) Mfugaji katika eneo la Halmashauri hataruhusiwa-
(a) kuchunga, kulisha au kunywesha maji mifugo katika maeneo yote ambayo hayakutengwa kwa ajili hiyo;
(b) kusafirisha mifugo kwa kuswaga barabarani;
(c) kuingiza mifugo katika eneo la Halmashauri bila kibali; na
(d) kupitisha mifugo katika maeneo ambayo hayakuidhinishwa na Halmashauri.

(2) Endapo mmiliki wa mifugo atakiuka kanuni ndogo ya (1), Halmashauri inaweza kukamata mifugo hiyo.

(3) Mmiliki wa mifugo itakayokamatwa chini ya kanuni ndogo ya (1) atapaswa kulipa faini kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(4) Endapo mifugo iliyokamatwa haitachukuliwa na mmiliki ndani ya siku saba tangu kukamatwa, Halmashauri itakuwa na haki ya kuuza mifugo kwa mnada baada ya kupata idhini ya mahakama, na fedha zitakazopatikana zitakabidhiwa kwa mmiliki baada ya kulipa faini inayodaiwa, gharama za kuhifadhi mifugo, gharama ya mahakama na gharama ya mnada.

(5) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (4), kabla ya kuuza mifugo kwa mnada Halmashauri itamjulisha mmiliki wa mifugo na umma kuhusu kusudio hilo.

(6) Endapo kutatokea kufa kwa mifugo kutokana na sababu yoyote, Halmashauri haitawajibika na ulipaji wa gharama zozote isipokuwa kama kifo kimesababishwa na uzembe wa watumishi wa Halmashauri.

*(b) Masharti kuhusu utunzaji wa misitu*

Wajibu wa mkazi

20.-(1) Kila mkazi atakuwa na wajibu wa kutunza miti kwenye maeneo yaliyohifadhiwa kwa ajili ya misitu

(2) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuchoma moto misitu iliyopo eneo la Halmashauri.

(3) Endapo moto utatokea katika eneo la Halmashauri, kiongozi wa eneo husika atawajibika kutoa amri kwa wakazi kuzima moto huo unapoonekana kuwa na madhara kwa maisha ya binadamu, mali na uharibifu wa mazingira katika eneo hilo.

(4) Kila mkazi atawajibika kushiriki kuzima moto iwapo atatakiwa kufanya hivyo na akishindwa kushiriki pasipo sababu ya msingi atakuwa ametenda kosa.

Ukataji miti

21.-(1) Mkazi hataruhusiwa kukata miti katika maeneo ya misitu iliyofadhiwa kwa ajili ya matumizi ya aina yoyote bila kupata kibali kutoka Halmashauri.

(2) Endapo kutakuwa na umuhimu kwa mkazi kuvuna miti kutoka kwenye msitu uliohifadhiwa, afisa misitu atatakiwa kuhakiki iwapo miti inayovunwa imekomaa na inafaa kwa ajili ya matumizi.

Uhifadhi wa uoto wa asili

22.(1) Halmashauri za vijiji zitawajibika kutenga na kutunza maeneo maalum kwa ajili ya hifadhi za misitu, uoto wa asili na viumbe hai.

(2) Endapo maeneo hayo yatakuwa yameharibiwa, Halmashauri za vijiji zitahakikisha wakazi wanapanda miti kwa ajili ya kurejesha uoto katika hali yake na kuzuia uharibifu wa mazingira.

Upandaji wa miti

23. (1) Kila mkazi atawajibika kupanda na kutunza miti katika eneo la makazi au shamba analomiliki.

(2) Kila taasisi ndani ya Halmashauri itapaswa kupanda miti ya kukinga upepo kuzunguka majengo ya taasisi husika.

(3) Upandaji wa miti kwa mujibu wa kanuni hii utazingatia ushauri wa mtaalamu wa Halmashauri.

*(c) Masharti kuhusu usimamizi wa vyanzo vya maji*

Wajibu wa kulinda

24.-(1) Halmashauri itawajibika kusimamia na kulinda vyanzo vya maji kwa kuweka mipaka, alama na

vyanzo vya maji

mabango ya ilani ya kuzuia uharibifu au uchafuzi katika maeneo hayo.

(2) Itakuwa ni wajibu wa Halmashauri kupanda miti isiyonyonya maji katika vyanzo vya maji.

(3) Itakua ni marufuku kwa mtu kulima, kukata miti, kuchunga mifugo katika umbali wa mita 60 kutoka kwenye chanzo cha maji au kufanya jambo lolote linaloharibu kwa namna yoyote chanzo cha maji na hifadhi ya mazingira.

(4) Itakuwa ni marufuku kwa mtu binafsi, kiwanda, taasisi, shirika kuelekeza maji taka kwenye chanzo cha maji.

Uchimbaji wa madini ya ujenzi

25-(1) Halmashauri itatenga maeneo maalum kwa ajili ya machimbo ya madini ya ujenzi kwa mujibu wa taratibu zitakazowekwa.

(2) Ni marufuku kwa mtu kuchimba madini ya ujenzi katika eneo la makazi ya watu, maeneo yaliyohifadhiwa kando kando ya mito, ndani ya mto, bwawa au katika maeneo yasiyoruhusiwa isipokuwa kwa ruhusa maalumu ya Halmashauri.

*(d)Masharti kuhusu kilimo*

Taratibu za kilimo

26. Mtu atakayetaka kuendesha shughuli za kilimo katika eneo la Halmashauri atatakiwa kuzingatia taratibu za kilimo zitakavyotolewa na Halmashauri.

Wajibu wa mkulima

27.-(1) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote-

(a) kulima katika miteremko, karibu au katika vyanzo vya maji au maeneo oevu yaliyotengwa, kandokando au kwenye kingo za vyanzo vya maji pasipo kuzingatia kanuni bora za kilimo;

(b) kutumia ardhi iliyotengwa kwa ajili ya kilimo kufanya shughuli nyingine isiyohusiana na kilimo; na

(c) kusafisha shamba kwa njia ya kuchoma moto isipokuwa kwa kibali cha Halmashauri na muda ulioruhusiwa.

(2) Mtu aliyepata kibali cha kuchoma moto atatoa taarifa ya siku mbili kabla ya kuchoma moto kwa majirani

walioko katika eneo analotaka kuchoma na ataweka njia za kuzuia moto kusambaa maeneo mengine.

(3) Halmashauri itakuwa na wajibu wa kusimamia shughuli za kilimo na kuzuia kilimo cha kuhamahama na kuhimiza kilimo cha mzunguko.

Matumizi ya viuatilifu

27. Halmashauri kwa kushirikiana na mamlaka husika za udhibiti wa viuatilifu zitaelekeza matumizi sahihi ya viuatilifu hivyo, na kufanya ukaguzi ili kubaini viuatilifu ambavyo ni hatarishi kwa afya ya binadamu na mazingira.

## SEHEMU YA NNE
## MASHARTI YA JUMLA

| | |
|---|---|
| Uteuzi wa wakala | 28.-(1) Halmashauri inaweza kuteua wakala kwa ajili ya kutekeleza jukumu lolote chini ya Sheria Ndogo hii. |
| | (2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa kanuni hii atawajibika kwa Halmashauri kwa mujibu wa mkataba baina ya wakala na Halmashauri. |
| | |
| Ushirikishaji wa jamii | 29. Halmashauri inaweza kushirikisha jamii kwa kuingia mkataba na mtu binafsi, taasisi, kikundi binafsi au asasi za kiraia, ndani ya Halmashauri katika ngazi ya kitongoji, kijiji, kata au wilaya katika kuboresha bustani, eneo la wazi na uhifadhi wa mazingira. |
| | |
| Makosa na adhabu | 30. Mtu yoyote ambaye- |
| | (a) atamzuia Mkurugenzi, afisa mwidhiniwa au wakala kutekeleza masharti ya Sheria Ndogo hii; |
| | (b) atashawishi au kusababisha mtu mwingine kutotekeleza masharti ya Sheria Ndogo hii; au |
| | (c) atakiuka masharti yoyote ya Sheria Ndogo hii, |
| | anatenda kosa na akipatikana na hatia atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini na isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichopungua miezi sita na kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote. |
| | |
| Kufifilisha kosa | 31. Mkurugenzi anaweza kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii kiasi |

| | |
|---|---|
| | kisichozidi shilingi laki mbili iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kujaza fomu maalum kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili . |
| | |
| Kufutwa kwa TS Na. 20 la 2016 | **32**. Sheria Ndogo ya Hifadhi ya Mazingiraa na Vyaanzovya Maji ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa inafutwa. |

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 19(3))*

VIWANGO VYA MALIPO YA KUHIFADHI MIFUGO ILIYOKAMATWA NA HALMASHAURI

| Na | Aina ya Mifugo | Kiwango cha malipo kwa siku kwa kila mfugo (Tsh.) |
|---|---|---|
| 1. | Mbuzi | 5000 |
| 2. | Ng'ombe | 5000 |
| 3. | Kondoo | 5000 |
| 4. | Punda | 5000 |
| 5. | Mbwa | 2000 |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 31)*

FOMU YA KUKIRI KOSA

Mimi………………………………………………………NAKIRI KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ……………………………………….. ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa, kwamba mnamo tarehe …… ya mwezi ……. Mwaka …… nilitenda kosa kwa kukiuka masharti ya kanuni ya .…… ya Sheria Ndogo ya Afya, Usafi na Hifadhi ya Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa ya Mwaka, 2024.

NAKUBALI kulipa kiasi cha shilingi.......... cha ada ninayodaiwa pamoja na faini ya shilingi.........

NATHIBITISHA KWAMBA, maelezo niliyotoa hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa MIMI MWENYEWE na kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu.

Leo hii tarehe………….ya mwezi…………..… mwaka 20…………….
Jina……………………………….....
Saini……….......…………………......

MBELE YA MKURUGENZI

Jina:………………….....................................
Saini:…………………..…..............................
Tarehe:.............................................................

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hii kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Baraza la Madiwani wa Halmashauri uliofanyika mnamo tarehe 9/11/2023 mbele ya:-

HANAN M. BAFAGIH,
*Mkurugenzi Mtendaji*,
*Halmashauri ya Wilaya Kilwa*

MHE. ISSA B. MATEKA,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya*

L.S

**NAKUBALI**,

Dodoma
29 Oktoba,2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi-OR-TAMISEMI*